# KUWEZESHA WANAWAKE

MRADI ULIYOFANYWA NA CCCEP | MUHTASARI NAMBA 3 | SEPTEMBA 2024



## KUWEZESHA WANAWAKE NI NINI?

Lengo la Maendeleo Endelevu namba 5 (SDG5) linahusu kufanikisha usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake na wasichana wote. Lakini, je, uwezeshaji unamaanisha nini na unavyokuwa katika muktadha tofauti, na tunawezaje kulifanikisha?

Ufafanuzi unaokubalika juu ya maana ya kuwawezesha wanawake ni "mchakato ambao wale waliokosa uwezo wa kufanya maamuzi muhimu kuhusu maisha yao wanapata uwezo huo" (Kabeer, 1999).

Uwezeshaji wa wanawake unaweza kueleweka kama mchakato unaoendelea kwa muda, ambapo wanawake hujiwekea malengo na kukuza uwezo wao wa kufanya maamuzi kuhusu maisha yao na matokeo wanayotaka kuyafikia. Hivyo, unahusiana kwa karibu na dhana ya matamanio – ambapo ni muhimu kuelewa malengo, chaguo, na matamanio ya wanawake kutoka kwa makundi na maeneo mbalimbali.

MBINU ZA MAENDELEO

Mbinu za kawaida za kuwawezesha wanawake zinajikita katika kukuza hisia ya thamani ya mwanamke, uwezo wake wa kufanya maamuzi kuhusu maisha yake mwenyewe, na haki yake ya kushawishi mabadiliko ya kijamii kwa faida yake na ya wengine.

Mara nyingi huwahamasisha wanawake kuchukua jukumu kubwa zaidi katika kufanya maamuzi – iwe katika kaya, jamii, au katika maeneo ya masoko. Kukuza ushiriki wa wanawake katika vikundi na katika siasa – hasa katika nafasi za uongozi – ni kipengele kingine muhimu katika mbinu za maendeleo za kuwawezesha wanawake.

Hata hivyo, kuwawezesha wanawake ni dhana tata inayoweza kumaanisha mambo tofauti kwa watu tofauti, na inatofautiana kulingana na maeneo na muktadha wa kitamaduni. Hii ina maana kwamba ni vigumu kutoa ufafanuzi na kupima – na wataalamu wanahitaji kuwa makini kutokuweka dhana zao wenyewe kuhusu maana na sura ya uwezeshaji wa wanawake.

## KUPIMA UWEZESHAJI WA WANAWAKE

Kupima uwezeshaji wa wanawake kunahusisha kutathmini uwezo wao wa kufanya maamuzi, rasilimali walizo nazo, na mafanikio waliyoyapata. Mbinu za kawaida za kupima zinaweza kugawanywa katika makundi kadhaa:

1) **Viashiria vya Kiuchumi –** upatikanaji na udhibiti wa rasilimali zinazozalisha kama kipato, ardhi, na mali nyingine
2) **Viashiria vya Elimu –** upatikanaji wa elimu, mafunzo, na huduma za karibu, na upatikanaji wa taarifa
3) **Viashiria vya Kijamii na Kitamaduni** – ushiriki katika mitandao ya kijamii na mashirika, uhuru wa kuhama
4) **Viashiria vya Kisiasa na Kisheria** – ushiriki katika uongozi wa serikali na kamati mbalimbali
5) **Viashiria vya Afya na Ustawi** – upatikanaji wa huduma za afya na lishe
6) **Viashiria vya Matumizi ya Muda na Kazi** – ukubwa wa kazi na utengaji wa muda, mgawanyo wa kazi kwa jinsia
7) **Viashiria vya Kisaikolojia –** kujiamini, hisia ya uwezo wa kuchukua hatua (inahusu uwezo wa mtu kujiona kuwa na nguvu ya kufanya maamuzi na kuchukua hatua katika maisha yake)

## MAMBO YA KUDHANIA KUHUSU UWEZESHWAJI: KUTAMBUA NA KUELEWA UDHOEFU

### DHANA ZA KIUCHUNGUZI

Kimsingi, uwezeshaji unabadilika kwa kutegemea muktadha. Ingawa mifumo mingi ya dhana ya uwezeshaji inalenga mtu binafsi, mara nyingi haizingatii umuhimu wa mshikamano wa kijamii, hatua za pamoja, na msaada wa pande zote katika mchakato wa kuwezesha.

Dhana nyingi za uwezeshaji wa wanawake zinatokana na maoni ya Kimagharibi kuhusu ubinafsi, uhuru wa mtu, na kujitegemea. Maadili haya huenda yasiwe yanayofaa kwa tamaduni zisizo za Kimagharibi, ambako kuna kanuni tofauti za kijamii na kijinsia.

Mara nyingi kuna msisitizo mkubwa juu ya uwezeshaji wa kiuchumi - kama vile kuongeza kipato na upatikanaji wa rasilimali za kifedha - kwa gharama ya nyanja zingine za uwezeshaji. Nguvu za kiuchumi si lazima zitafsiriwe kuwa wakala au mamlaka ya kufanya maamuzi.

### DHANA ZA UPIMAJI

Kudhani kwamba uwezeshaji unaweza kupimika au kuhesabika kunahitaji ufafanuzi wa dhana ya uwezeshaji na maadili ambayo yatatumika kama msingi wa kupimia. Hata hivyo, sio mbinu moja inayofaa kila mahali kuakisi kikamilifu upekee wa uwezeshaji wa wanawake katika muktadha tofauti wa kitamaduni na kijiografia.

Maana na mitazamo ya eneo kuhusu uwezeshaji inaweza kutofautiana sana.

Kwa kuwa uwezeshaji ni **mchakato**, vipimo vyake vinaweza kuonyesha hali ya muda tu na kushindwa kufuatilia mabadiliko yanayotokea kwa muda mrefu.

Aidha, kuzingatia taarifa za mtu binafsi au ngazi ya kaya kunaweza kushindwa kuakisi kikamilifu mienendo ya madaraka na mahusiano ya kijinsia ndani ya famili au jamii

### KUELEWA UTOFAUTI

Wanawake si kundi lenye sifa moja. Wanatofautiana kwa maadili, matamanio, na vikwazo vinavyoathiri uzoefu wao wa uwezeshaji. Mambo kama kabila, umri, dini, na hali ya ndoa huathiri na kuchangia tofauti hizi.

'Nguvu' si kitu ambacho wanawake hupata au kupoteza tu; inakuwepo na inafanya kazi ndani ya mahusiano. Ina badilika badilika, ugombewa na mara nyingi hutekelezwa kwa njia za hila.Kuna aina mbalimbali za nguvu zinazoonyesha vipimo tofauti vya jinsi watu binafsi au makundi yanavyotekeleza.

Uwezeshaji haupatikani mara moja; ni mchakato unaochukua muda mrefu-Uwekezaji wa muda mfupi mara nyingi hauwezi kuleta mabadiliko yanayoonekana au yanayoweza kupimika. Kwa uwezeshaji endelevu, ni muhimu kuzingatia mabadiliko ya muda mrefu ya kimuundo.

## TAFITI ZA FOSTA-AFYA

FoSTA-AFYA imekuwa ikichunguza uelewa na uzoefu wa uwezeshaji katika Mkoa wa Tanga, Tanzania. Baadhi ya matokeo ya awali ni:

- Wanawake wakulima wadogo wadogo wengi wanachukulia uwezeshaji kama kupokea mikopo – mara nyingi kupitia vikundi. Uwezeshaji wa aina hii unaonekana kama kitu wanachopokea kutoka kwa serikali na mashirika ya maendeleo. Hata hivyo, kuna changamoto zinazotokana na jinsi wanawake wanavyopata uzoefu wa uwezeshaji:
    - Ushiriki wa wanawake kwenye vikundi unaweza kuzuiliwa na ukosefu wa fedha au uhusiano wao na waume zao, na mara nyingine vikundi havifanyi kazi kama ilivyotarajiwa (angalia muhtasari namba 4). Aidha, mikopo yenye riba kubwa inaweza kuwa vigumu kulipwa, na kusababisha migogoro ndani ya vikundi na nyumbani. Hali hii hufanya upokeaji na utekelezaji wa uwezeshaji kuwa changamoto.
- Baadhi ya wanawake wanaona uwezeshaji kama kujitegemea kiuchumi – lakini si wote. Wanawake wengine wanapendelea kuchangia kwenye kipato cha kaya na wenzi wao, na kukaa pamoja ili kuamua matumizi yake.
- Wanawake wengine wanatafsiri uwezeshaji kama elimu – katika kilimo na katika kuelewa haki zao. Mafunzo haya, hata hivyo, yanaweza kuathiri jinsi wanavyotafsiri dhana ya uwezeshaji.
- Kwa ufupi, wanawake tofauti wanauelewa uwezeshaji kwa njia tofauti.

### Kuelewa Nguvu na Wakala

**Nguvu Ndani:** Inaakisi sauti ya ndani ya mtu, heshima ya nafsi, au kujiamini.

**Nguvu ya Kufanya:** Inahusisha uwezo wa mtu kufanya maamuzi kwa maslahi yake binafsi, kama vile kudhibiti kipato/rasilimali au maamuzi yanayohusiana na huduma za kifedha.

**Nguvu ya Pamoja:** Nguvu inayotokana na kushirikiana na wengine – kwa mfano, kupitia vikundi.

Kazi ya uwezeshaji inapaswa kuhoji zaidi ya dhana ya kwamba "wanaume wana nguvu dhidi ya wanawake." **Nguvu za kimuundo** zimejikita katika mifumo ya kijamii, kisiasa, na kiuchumi, na huathiri ni nani anayepata rasilimali, fursa, na haki, na ni nani anayekosa.

## MAPENDEKEZO

- Chukua muda kukaa na jamii ili kusikiliza na kuelewa maana ya uwezeshaji kwao. Hii itasaidia kuhakikisha kuwa malengo ya mradi yanaendana na maadili na mahitaji ya jamii, na kusaidia katika kubuni kwa pamoja mbinu sahihi za kupima.
- Tambua kwamba uwezeshaji unaweza kueleweka na kuonekana tofauti na watu tofauti. Kwa hivyo, ubunifu, utekelezaji, na ufuatiliaji wa mradi unapaswa kuzingatia hayo.
- Kumbuka kwamba uwezeshaji ni mchakato, zana hizi zinaweza kuhitaji kurekebishwa wakati wowote wa kipindi cha utekelezaji mradi.
- Fikiria jinsi mbinu za ushirikishwaji zinavyoweza kutumika kusaidia kujenga uwezo na uwezeshaji ili kuleta matokeo endelevu.

Prepared and disseminated through collaboration with the ESRC Climate Change Centre for Economics and Policy Legacy project led by UoLeeds and Tanzania Forest Conservation Group

To find out more about the project, please visit fosta-health.eu